

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA TATU

Kikao cha Thelathini na Mbili – Tarehe 20 Mei, 2021

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa, tukae.

Katibu.

NDG. ZAINAB ABDALLAH – KATIBU MEZANI:

TAARIFA YA SPIKA

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, Taarifa ya Mheshimiwa Spika inayotolewa chini ya Kanuni ya 39(2) ya Kanuni zetu za Kudumu za Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa sana anawatangazia Waheshimiwa Wabunge na kuwataarifu kwamba Mbunge mwenzetu, Mheshimiwa Khatib Said Haji, Mbunge wa Jimbo la Konde kupitia Chama cha ACT Wazalendo amefariki leo Alhamisi tarehe 20 Mei, 2021. Amefariki majira ya saa 11:40 alfajiri katika Hospitali ya Muhimbili alipokuwa akipata matitabu.

Waheshimiwa Wabunge, mazishi ya ndugu yetu Mheshimiwa Khatib Said Haji, yatafanyika leo saa 10:00 alasiri huko Pemba. Taratibu zinafanyika ili kupata Waheshimiwa

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Wabunge watakao kwenda kuliwakilisha Bunge katika mazishi haya huko Pemba.

Na Wabunge watakaokwenda kutuwakilisha ni wale ambao wako Dar es Salaam katika kipindi hiki, wengi wao walikuwa wameenda kwa ajili ya shughuli ya Kitaifa ambayo ipo siku ya leo inayohusu Bomba la Mafuta. Kwa hiyo, wako Dar es Salaam kati ya hao wachache wetu wataenda kutuwakilisha na kwa taratibu zetu kwa wale ambao wapo kule basi wataangalia uwakilishi wa vyama humu ndani na uwakilishiwa mambo mengine kama ambavyo huwa tunafanya katika taratibu zetu.

Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni ya 173 ambayo inataka kuahirisha shughuli za Bunge kunapotokea kifo cha Mbunge mwenzetu wakati Bunge likiwa kwenye shughuli zake, sasa naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho, siku ya Ijumaa tarehe 21 Mei, 2021 saa 3:00 asubuhi ili Waheshimiwa Wabunge tupate muda wa maombolezo kwa ajili ya huyu mwenzetu ambaye ametutoka.

Mungu ailaze roho ya Marehemu mahali pema peponi, Amina.

*(Saa 3:04 Asubuhi Bunge Lilahirishwa hadi Siku ya Ijumaa,
Tarehe 21 Mei, 2021 Saa Tatu Kamili Asubuhi)*